

Swahili

Manispaa itawasiliana nawe kwa ujumbe mfupi kabla ya kupokea chanjo dhidi ya korona

Wakati wako wa kupewa chanjo, manispaa itawasiliana nawe kwa ujumbe mfupi. Ikiwa huwezi kupatikana kwa njia ya simu, utapokea barua kwenye posta. Hupaswi kuwasiliana na manispaa mwenyewe.

Unapoambiwa kuwa ni wakati wako wa kupewa chanjo, unaweza kwenda kwenye kalenda ya chanjo ya manispaa ya Trondheim (kiungo) ambapo unaweza kuweka miadi. Lazima upewe chanjo mara mbili na lazima uweke miadi kila wakati.

Chanjo ni bila malipo.